**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA UFAULU WA MTIHANI WA TAIFA KIDATO CHA M2024 KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA MLIMBA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mlimba, ndg. Jamary Idrisa Abdul, anajivunia kutoa taarifa ya uchambuzi wa matokeo ya mtihani wa Taifa wa kidato cha nne kwa mwaka **2024** kwa shule zake zote **25** zilizo fanya mtihani huo, ambapo ufaulu wa jumla ni **95.33%** huku watahiniwa **2611** kati ya **2741** wakiwa wamefaulu, miongoni mwao wavulana **1,308** kati ya **1,341** wamefaulu, na wsichana **1,303** kati ya **1400** wamefaulu.

Hata hivyo, ufaulu umeonesha kushuka kwa **3.71%** ukilinganisha na matokeo ya mwaka **2023**, ambapo ufaulu wa jumla ulikuwa **99.04%.**

Ingawa kumekuwepo na upungufu katika ufaulu, juhudi za pamoja kutoka kwa wadau mbalimbali, ikiwa ni pamoja na walimu, wanafunzi, wazazi, na jamii kwa ujumla zimeweza kusaidia kuleta mafanikio makubwa ya kitaaluma katika shule nyingi za Halmashauri ya Mlimba.

**Shule Zilizofanya Vizuri Zaidi:**

Katika tathmini ya matokeo hayo ya mwaka **2024**, shule **11** zimefaulu kwa asilimia **100**, jambo ambalo linaonesha jitihada za walimu na wanafunzi katika shule hizi kuzingatia masomo kwa umakini na ufanisi. Aidha, shule tisa zimefaulu kwa asilimia kati ya **91** hadi **98**, tatu zimefaulu kwa asilimia kati ya **80** hadi **82** na shule moja imepata ufaulu wa **76.4%.**

Hata hivyo, Divisheni ya Elimu ya Sekondari ya Halmashauri tayari imeshaazimu kuweka mkakati wa kuhakikisha kiwango cha ufaulu kinaimarika katika shule hizo hadi kufikia ufaulu wa asilimia **100** kwa shule zake zote.

**Masomo Yaliyofanya Vizuri:**

Masomo ya Sanaa yameonesha mafanikio makubwa ukilingansha na masomo ya sayansi katika matokeo hayo. Hii inaifanya Halmashauri kuendelea kuweka mkazo zaidi katika masomo ya sayansi kwani ni ya muhimu pia katika maendeleo ya taifa hasa nyakati hizi za mapinduzi ya teknolojia.

**Mikakati Iliyotumika Kufikia Ufaulu Huu:**

Ufaulu wa jumla wa **95.3%** ambao halmashauri imeupata, umechangiwa na mikakati mbalimbali iliyotekelezwa na Halmashauri pamoja na shule husika. Baadhi ya mikakati hiyo ni:

1. Chakula shuleni: kuhakikisha chakula cha mchana kinapatikana shuleni kwa wanafunzi wote na hasa wa madarasa ya mitihani kumechochea uwezo wa wanafunzi kujifunza na kushiriki kikamilifu darasani,
2. Masomo ya ziada: Shule zimeweka muda wa ziada kwa ajili ya wananfunzi kujifunza na walimu wamekuwa wakijitoa kwa dhati kufundisha nyakati hizo.
3. Mitihani ya ujirani mwema na mitihani ya mara kwa mara ndani shule: shule zimekuwa zikifanya mitihani ya mara kwa mara ya ndani na ya nje ya shule na hii imekuwa ikiongeza ari ya wanafunzi kutaka kufanya vizuri zaidi katika mitihani,

4. Michezo kwa wanafunzi: shule zimekuwa zikihimiza michezo ya ndani na ya ujirani ili kuchangamsha bongo za wanafunzi na kuleta matokeo chanya katika ufaulu,
5. Motisha kwa walimu: Halmashauri imekuwa ikiwapatia zawadi walimu wanao fanya vizuri katika taaluma na hii imekuwa ikichochea hamasa ya walimu katika ufundishaji, na
6. Ufuatiliaji: Halmashauri kupitia maafisa elimu wake, imekuwa ikifanya ufuatiliaji wa mara kwa mara, wa ufundishaji na ujifunzaji katika shule zote, hali ambayo imekuwa ikichangia walimu kufanya kazi yao kwa uweledi na ufanisi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Mlimba, ndg. Jamary Idrisa Abdul anasema uwepo wa vyumba vya madarasa vya kutosha pamoja na samani zake (viti na meza), hosteli kwa ajili ya wanafunzi waishio mbali na shule, majengo mazuri na ushirikiano mzuri baina ya wazazi na walimu pia vimechangia sana kuimarika kwa taaluma na ufaulu shuleni.

Mkurugenzi Jamary ameendelea kumshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mhe. Dkt.Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuleta fedha nyingi katika Halmashauri kujenga miundombinu mbalimbali shuleni na kuimarisha mazingira ya ujifunzaji na ufundishaji.

**Changamoto Zinazokwamisha Ufaulu:**
Licha ya mafanikio haya, hali ya utoro na uelewa mdogo wa baadhi ya wazazi na walezi kuhusu umuhimu wa elimu vinabakia kuwa changamoto kubwa inayokwamisha ufaulu miongoni mwa wanafunzi, ambapo baadhi ya wazazi wamekuwa hawawajibiki vya kutosha ikiwa ni pamoja na kutochangia kwa ukamilifu huduma ya chakula cha mchana kwa watoto wao.

Hata hivyo, Halmashauri inaendelea kutoa elimu kwa wazazi na jamii kupitia vikao na madawati ya ushauri nasaha kwa wanafunzi ili kuweza kuboresha hali ya elimu na kuhakikisha watoto wote wanapata fursa ya kufaulu vizuri.

Vilevile, kwa mwaka huu, Halmashauri tayari imekwisha kuanza mchakato wa kuwabaini mapema na kuwawekea mkakati madhubuti wa kuwaimarisha wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mitihani ya Taifa ya kidato cha pili, cha nne na cha sita, ambao kuelewa kwao ni taratibu (slow learners).

Yote hayo yanatazamiwa kusaidia kuongeza ufaulu miongoni mwa wanafunzi hatimaye Halmashauri itatimiza azma yake ya kufuta ziro na baadae kufuta ufulu wa daraja sifuli katika shule zake zote.

**MWISHO**

**Imetolewa na,**
**Kitengo cha Mwasiliano ya Serikali,**
**29.01.2025**